# MWONGOZO WA MZAZI

YouthCity
Elementary K-6

2025-2026

Wapendwa Wazazi na Walezi wa YouthCity,

Karibu kwenye mpango wa Baada ya shule wa YouthCity wa 2025-26! Katika miezi kadhaa iliyopita, timu zetu zimekuwa na shughuli nyingi za kupanga na kujitayarisha kwa mpango wa mwaka mzima uliyojaa burudani na tunafurahi kuwa wewe na familia yako mtajiunga nasi.

Mwaka huu, vijana wa umri wa shule kutoka Salt Lake City yote walioandikishwa kwenye mpango wa Baada ya shule wa YouthCity watahusika katika shughuli halisi za kujifunza kielimu ili kujifunza dhana za STEM, kujifunza kuhusu afya na siha, kuhusika katika miradi ya huduma kwa jumuiya, kutembelea vyuo na vyuo vikuu vya karibu, na kukuza ujuzi wa msingi wa kifedha. Kama awali, wafanyakazi wa YouthCity wanapanga madarasa, shughuli na safari za kielimu zilizoundwa kugundua washirika wa jumuiya na maeneo ndani ya jiji letu nzuri, kuongeza ujifunzaji kwa njia mpya, kuwahamasisha vijana kujaribu mambo mapya na kupanua miunganisho yao ya kijamii na makundi ya wanarika. Vijana watashiriki katika safari za kielimu za kila mwezi na pia kujifunza kuhusu sanaa na ubunifu, spoti na burudani, stadi za maisha na madarasa ya STEM. Katika kuendeleza mafanikio ya miaka michache iliyopita, tunafuraha kuendelea na mpango wetu mpya wa uongozi wa marika na hivi karibuni tutawatambua watoto 6 watakaohudumu katika Baraza la Uongozi la YouthCity. Utakuwa mwaka wa masomo wenye mafanikio!

Wafanyakazi wetu wenye mafunzo ya hali ya juu, motisha na huruma wanafuraha kuanza kushirikiana nawe na watoto wako. Hapa chini tumetoa maelezo utakayohitaji kuhakikisha tuna mwaka wa masomo ulio salama na mafanikio. Tunakushukuru kwa kutuaminia na watoto wako na jua kwamba tunafurahia kushirikiana na kila mmoja wenu. Tafadhali usisite kuwasiliana nasi ukiwa na hitaji.

Natuma salamu zangu za dhati!

Angel Gomez
Mkurugenzi Mshirika - Kitengo cha Vijana na Familia
Angel.Gomez@slc.gov

### *SAA ZA KAZI*

Mipango ya YouthCity hufuata kalenda ya Wilaya ya Shule ya Salt Lake City na huendesha mipango katika siku ambazo shule zimefunguliwa. Wakati shule za Wilaya ya Shule ya Salt Lake City zimefungwa, hatuendeshi mipango ya YouthCity.

Kwa kutumia magari ya jiji, wafanyakazi wa mpango huwasafirisha watoto kutoka shule zao hadi kwenye maeneo ya YouthCity. Kwa kushirikiana na viongozi wa shule, wafanyakazi husubiri nje ya kila shule katika eneo lililotengwa. Pindi kila kijana anapotambuliwa, gari linaondoka kwenye mali ya shule na kufika katika YouthCity.

Ikiwa wazazi wanapanga kuwachukua wanafunzi, wanahitaji kuchukuliwa kutoka kwenye mpango kufikia saa 5:20 pm. Wafanyakazi wataanza kuwarudisha kila siku saa 5:20 pm. Ikiwa mwanafunzi anarudishwa nyumbani na mfanyakazi wa YouthCity, mtarajie kufika kati ya saa 5:30 na saa 6:00 pm.

### *ADA ZA MPANGO*

Ada za mpango zinaamuliwa kulingana na ukubwa na mapato ya familia. Tafadhali angalia kifurushi ya usajili kwa maelezo zaidi. Ada zote zinazodaiwa za mpango lazima zilipwe kikamilifu kabla ya mwanafunzi kuhudhuria mpango. Kama tahadhari ya kiafya, tunahimiza familia kulipa ada za mpango mtandaoni. Hundi na hawala za fedha zinakubalika kama inavyohitajika. Wasimamizi Wakuu wa Mpango wa Jamii na Wasimamizi wa Mipango ya Jamii watawasiliana na familia ili kutoa maelezo kuhusu ada zozote za mpango zinazodaiwa.

## TAREHE MUHIMU

| | |
|---|---|
| Jumanne, Agosti 19 | Siku ya kwanza ya Mpango wa Baada ya Shule wa YouthCity wa 2025-2026 |
| Jumatatu, Septemba 1 | Siku ya Wafanyakazi - Hakuna YouthCity |
| Ijumaa, Septemba 26 | Hakuna Shule - Hakuna YouthCity |
| Oktoba 16 hadi 20 | Mapumziko ya Msimu wa Mapukutiko - Hakuna YouthCity |
| Novemba 26 hadi 28 | Sikukuu ya Siku ya Kutoa Shukrani na Hakuna YouthCity |
| Desemba 22 hadi Januari 2 | Mapumziko ya Msimu wa Baridi - Hakuna YouthCity |
| Jumatatu, Januari 19 | Sikukuu ya Martin Luther King, Jr. - Hakuna YouthCity |
| Jumatatu, Februari 16 | Sikukuu ya Rais - Hakuna YouthCity |
| Machi 31 hadi Aprili 4 | Mapumziko ya Msimu wa Machipuko - Hakuna YouthCity |
| Aprili 6 hadi 10 | Mapumziko ya Msimu wa Machipuko - Hakuna YouthCity |
| Ijumaa, Mei 22 | Siku ya mwisho ya Mpango wa Baada ya Shule wa YouthCity wa 2025-2026 |

## MAELEZO YA MAWASILIANO YA MPANGO

| *Mipango ya YouthCity ya Chekechea hadi Gredi ya 6* | *Kiongozi wa Mpango* | *Simu ya Mpango* | *Barua pepe ya Mawasiliano* |
|---|---|---|---|
| Central City Rec. Center Chekechea hadi gredi ya 6 | Erica Andino | 801-381-6836 | Erica.Andino@slc.gov |
| Fairmont Park Chekechea hadi gredi ya 6 | Lauren Underwood | 801-573-6519 | Lauren.Underwood@slc.gov |
| Liberty Park Chekechea hadi gredi ya 6 | Jess Ung | 801-558-8223 | Jess.Ung@slc.gov |
| Fairpark Chekechea hadi gredi ya 6 | Michael Vargas | 385-495-6519 | Michael.Vargas@slc.gov |
| Ottinger Hall Chekechea hadi gredi ya 6 | Connie Paredes-Pozas | 801-573-1349 | Connie.Paredes-Pozas@slc.gov |
| Sorenson Unity Center Gredi ya 3 hadi 6 | Lola Paredes | 801-879-9678 | Dolores.Paredes@slc.gov |
| Sorenson Multi-Cultural Center Chekechea hadi gredi ya 2 | Fernando Puga | 385-282-9933 | Fernando.Puga@slc.gov |

## MPANGO WA BAADA YA SHULE WA 2025 - 2026

Kama miaka ya awali, YouthCity itatoa ujuzi mbalimbali unaolingana na umri kupitia shughuli halisi zinazolenga Sanaa na Ubunifu, Spoti na Burudani, Stadi za Maisha, STEM na uchunguzi wa nje. Madarasa na shughuli zimeundwa kuchochea kujifunza na kukuza miunganisho ndani ya jumuiya.

Mwaka huu wa masomo tunafurahi kulenga mafunzo yetu kwa mada zifuatazo za vipindi.

| *Tarehe* | *Mada za Kipindi* | *Maeneo Yanayolengwa ya Mafunzo ya Kijamii na Kihisia (SEL)* |
|---|---|---|
| Agosti 19 hadi 29 | Wiki ya Makaribisho | Maana ya Uwezo wa Mtu Mmoja ni nini? |
| Msimu wa Mapukutiko 1<br>Septemba 1 hadi Oktoba 31 | Kongamano la Sayansi | Diplomasia, Kujitambua, Uanuwai na Ujumuishaji |
| Msimu wa Mapukutiko 2<br>Novemba 2 hadi Desemba 19 | Kujitolea kwa Afya | Haki, Utumishi, Uelewa, Kufikiri kwa Makini |
| Msimu wa Baridi<br>Januari 5 hadi Machi 6 | Waleta Tofauti na YouthCity University | Huruma, Ustahimilivu, mawasiliano, Utatuzi wa Matatizo |
| Msimu wa Machipuko<br>Machi 9 hadi Mei 22 | CityVille | Huruma, Ustahimilivu, mawasiliano, Utatuzi wa Matatizo |

### *Safari za Kielimu:*

Kila wiki, vijana watatembelea majumba ya makumbusho, biashara, na vivutio mbalimbali vya eneo ili kusaidia kukuza miunganisho ya maana kwa jamii yetu. Wafanyakazi wa mpango wamepanga na kuunda safari maalum kwa uangalifu ili kuwasaidia watoto wa YouthCity kufanya miunganisho ya kimasomo, kujenga urafiki, na kukuza ujuzi wa kutatua matatizo unaolingana na umri. Tahadhari zote za afya zitazingatiwa ili kusaidia kuwaweka washiriki wa mpango, wafanyakazi wa mpango na wanajamii salama. Kila mwezi, Wasimamizi Wakuu wa Mipango ya Jamii watatoa kwa familia kalenda ya matukio ikijumuisha safari za kielimu na shughuli.

### *Miongozo ya Afya na Usafishaji:*

Kulingana na miongozo ya afya na usalama iliyotolewa na Idara ya Afya ya Utah, tahadhari zifuatazo za afya zitajumuishwa katika mpango wa Baada ya shule wa YouthCity wa 2025-26. Vijana ambao hawatafuata miongozo hii wataondolewa kwenye mpango.

Wafanyakazi wa mpango watafuata ratiba madhubuti ya usafishaji ili kutakasa sehemu za jengo siku nzima. Kila kituo kitasafishwa kwa kina kila siku baada ya saa za mpango. Milango ya jengo itafungwa wakati wa saa za mpango.

### *Kunawa mikono:*

Kunawa mikono mara kwa mara na kwa uthabiti huhitajika siku nzima na kuhimizwa wakati wa mapumziko na nyakati za kubadilisha shughuli. Watu wote watahitajika kunawa mikono wanapoingia ndani ya jengo, baada ya kwenda msalani, na kabla ya kula milo na vitafunio vyote.

### *Usafishaji na Utakasaji:*

Maeneo yote ya YouthCity yana vifaa vya usafishaji na utakasaji ili kuhakikisha sehemu zinazoguswa sana zinasafishwa na kutakaswa baada ya kila matumizi. Tumeanzisha ratiba za kutakasa na kusafisha nafasi zetu ambazo zitakamilishwa kabla ya mpango kuanza, wakati wa mpango, na baada ya mpango. Vitana watahimizwa kusaidia kuweka nafasi hizi zikiwa safi na nadhifu. Majengo yote ya YouthCity yatasafishwa na kutakaswa kwa kina pindi mpango unapomalizika kila usiku.

### *Sera ya Ugonjwa:*

Ikiwa mtoto wako anaumwa, anapaswa kubaki nyumbani na asihudhurie mpango. Ikiwa mtoto atapata dalili wakati mpango unaendelea, wafanyakazi watamtenga mtoto huyo kwa usalama na kutoa huduma ya kwanza na utunzaji, watawasiliana na wazazi ili kuomba mtoto achukuliwe kutoka kwa mpango haraka iwezekanavyo. Viongozi wa Mpango watashirikiana na wazazi kufuatilia afya na dalili za mtoto ili kubaini ni lini mtoto anaweza kurudi kwenye YouthCity. Ikiwa mtoto wako hahudhurii shule kwa sababu ya maradhi, basi hapaswi kuhudhuria YouthCity. Tafadhali wasiliana na Msimamizi Mkuu wa Mipango ya Jamii ili kuripoti ikiwa mtoto wako hatahudhuria mpango.

### *Itifaki za Covid 19:*

Kulingana na maelekezo kutoka kwa viongozi wa Jiji, vijana na wafanyakazi watafuata miongozo ya afya inayopendekezwa ili kusaidia kudumisha afya na usalama ndani ya jumuiya yetu. Vijana na wafanyakazi wanaweza kuchagua kuvaa barakoa na YouthCity itatoa barakoa kama inavyohitajika. Maelezo na taarifa zaidi zitatolewa kama inavyohitajika.

### *Skuta, Baiskeli na Matumizi ya Uwanja wa Michezo:*

Vijana wanaweza kuendesha baiskeli na skuta katika nyakati za mpango wa YouthCity. Wakati wa saa za mpango, vijana watahitajika kuvaa helmeti wanapoendesha baiskeli, bao za mtelezo au skuta. Aidha, vifaa vya uwanja wa michezo vitaruhusiwa mradi hali ya afya ya jamii inazingatiwa.

### *Majeraha:*

Wafanyakazi wote wa YouthCity wamefunzwa jinsi ya kutoa Huduma ya Kwanza na Kuhuisha Moyo na Mapafu (CPR). Katika matukio ya majeraha ambayo yanaonekana kuwa madogo, huduma ya kwanza itatolewa ndani ya jengo. Katika hali mbaya zaidi, tutamjulisha mzazi haraka iwezekanavyo. Ikiwa ni muhimu, tutapiga simu au kuwasiliana na watu wazima wengine kwenye orodha ya mawasiliano ya dharura. Wafanyakazi watachukua hatua kulingana na uamuzi wao wa busara kwa ajili ya ustawi wa mtoto. Hii inaweza kujumuisha lakini sio tu: kuita gari la wagonjwa au kufanya CPR au kutumia mbinu zingine za Huduma ya Kwanza.

***Muundo wa Wafanyakazi wa YouthCity:***

Wafanyakazi wote wa YouthCity hupokea mafunzo ya muda usiopungua saa 25 kila mwaka. Mafunzo yanajumuisha ustawishaji wa vijana wanaobalehe, huduma ya kwanza, CPR, mbinu zinazofaa za nidhamu, ushughulikiaji wa chakula, mafunzo ya kutumia gari, kuendesha gari kwa kujilinda, kuzuia dhuluma dhidi ya watoto na mbinu bora katika uendelezaji wa mtaala. Wafanyakazi huunda mtaala kulingana na historia na tajriba yao. Wafanyakazi wote wamekamilisha uchunguzi wa kina wa historia yao unaofanywa na Ofisi ya Kutoa Leseni ya Matunzo ya Watoto.

***Kumleta na Kumchukua Mtoto Wako:***

Kila eneo la YouthCity limeundwa kwa ubunifu na mpangilio wa kipekee wa mpango. Tafadhali wasiliana na Msimamizi Mkuu wa Mipango ya Jamii uliyepewa ili ufahamu itifaki na maelekezo ya maegesho mahususi kwa eneo. Wafanyakazi wa YouthCity wanawajibika kwa watoto walioandikishwa kwenye mpango pindi kengele ya shule inapolia. Vijana wote wanapaswa kuchukuliwa saa 6:00 pm kila siku. Tafadhali onyesha kwenye kifurushi cha usajili ni kina nani walioidhinishwa kumchukua mtoto wako kutoka YouthCity. Wafanyakazi wa Program wamefunzwa kuwaachilia vijana kwa watu pekee walioidhinishwa waliotajwa kwenye fomu ya usajili.

***Wawasiliani wa Dharura:***

Wazazi/Walezi lazima watoe majina ya watu wote walioidhinishwa kumchukua mtoto wako, fomu ya kuondoka imejumuishwa katika nyenzo zetu za usajili. Tafadhali hakikisha umetaja watu wote walioidhinishwa kumchukua mtoto wako na uhakikishe kuwa wanaelewa itifaki za kumchukua mtoto zilizoelezwa hapa chini. Watu wazima ambao hawajulikani wataombwa waonyeshe utambulisho.

***Chakula na Lishe:***

YouthCity itatoa kitafunio chenye afya kila siku. Menyu huchapishwa ndani ya kila kituo na zinaweza kutolewa kwako ukiomba. Wazazi pia wanaweza kumpa mtoto wao kitafunio kila siku. Tafadhali hakikisha chakula ni tayari kula na HAKIHITAJI kuhifadhiwa kwenye jokofu au kupashwa joto kwa mikrowevu. Pia tunaomba uweke lebo kwenye chakula cha mwanafunzi wako inayoonyesha jina lake. Wanafunzi wanafaa kuja na chupa ya maji kila siku.

Ni wajibu wa mzazi/mlezi kujulisha mpango ikiwa mtoto wao ana mzio wowote. Mpango utatoa chaguo zinazofaa cha vitafunio kwa wanafunzi walio na mahitaji maalum ya lishe. Tafadhali onyesha kwenye fomu ya usajili ikiwa mtoto wako ana vikwazo kutokana na mzio.

***Maradhi:***

Vijana walio na dalili zozote zifuatazo, lakini sio tu hizi, hawapaswi kuhudhuria Mpango:

- Homa
- Kikohozi
- Upungufu wa pumzi
- Kuhara
- Kutapika
- Mafua na/au mwasho mkali wa koo
- Halijoto ya mwili inayozidi nyuzi 99
- Watoto na watu wazima wanaoonyesha mojawapo ya dalili hizi hawapaswi kuingia kwenye kituo na wanafaa kuwasiliana na mtoa huduma wao wa afya ili kubaini ikiwa dalili zinahusiana na COVID-19 au maradhi mengine. Ikiwa yeyote anayehusishwa na kituo, mwanafunzi au mfanyakazi atapimwa na kugunduliwa kuwa na COVID-19, kituo chetu kitahitajika kufungwa kwa muda.

Ikiwa mwanafunzi wako ataonyesha dalili za maradhi baada ya kufika kwenye kituo, tutamtenga na vijana wengine. Mtoto wako atafuatiliwa katika eneo tulivu. Ikiwa mwanafunzi wako ataugua wakati wa mpango, Viongozi wa Mpango watawasiliana nawe au mtu aliyeidhinishwa ili kumchukua mtoto wako kutoka kwa mpango mara moja. Ikiwa hatuwezi kumfikia mzazi, tutapigia namba za simu za mwasiliani wa dharura wa kijana.

***Dhuluma/Utelekezaji:***

Kama wataalamu wa matunzo ya watoto, tunahitajika kisheria kuripoti visa vyovyote vinavyoshukiwa vya dhuluma au kutelekezwa kwa watoto. Hatutasita kutafuta usaidizi kwa ajili ya mtoto yeyote.

***Dawa:***

YouthCity haitoi dawa kwa washiriki walioandikishwa.

***Chanjo:***

Kila mtoto anahitajika kupata chanjo zote zinazohitajika.

## *UTARATIBU WA MPANGO*

### *Matarajio ya Kitabia:*

YouthCity inatarajia watoto kutenda kwa heshima na kuwajibikia tabia zao wanapokuwa kwenye mpango. Tunawatarajia watoto kuheshimu wanafunzi wenzao, wafanyakazi na watu wazima wengine, vifaa, nyenzo na wao wenyewe. Ikiwa kijana wako hawezi kufikia matarajio haya, wafanyakazi wa mpango watatoa adhabu zinazofaa ili kupunguza tabia hiyo.

Wakati tabia mbaya inapoongezeka, watoto watapewa onyo la maneno na mfanyakazi ataelekeza tabia yao kwenye chaguo zenye tija zaidi. Ikiwa tabia hiyo mbaya itaendelea, adhabu za ziada zitatumika. Adhabu ni pamoja na kutengwa kwa muda mfupi, kutengwa kwa muda kamili kutoka kwa shughuli au darasa, kupoteza manufaa mengine ya mpango au kufanyika kwa mkutano na mzazi au mlezi wa mwanafunzi.

Katika hali ambapo tabia mbaya inaendelea kwa muda mrefu, mwanafunzi anaweza kusimamishwa kwenye mpango au katika hali iliyokithiri, kufukuzwa. Muda wa kusimamishwa huanzia siku 1 hadi 5. Kabla ya kusimamishwa, Viongozi wa Mpango, mwanafunzi, na mzazi watakutana na kukubaliana mpango unaofaa wa kusimamishwa. Mkutano na Msimamizi Mkuu wa Mpango wa Jamii wa kituo unahitajika kufanyika kabla ya mwanafunzi kurudi kwenye mpango.

Katika visa hivi vikali, YouthCity inahifadhi haki ya kusimamisha au kumfukuza mshiriki.

Mipango ya YouthCity hairuhusu KAMWE vurugu. Katika visa vya vurugu, vitisho vya vurugu, na uonevu, wanafunzi wanaweza kusimamishwa au kufukuzwa mara moja. Wazazi watapigiwa simu na kuombwa kumchukua mwanafunzi wao haraka iwezekanavyo. Uonevu wa kijamii, utengaji au uonevu wa mtandaoni kwenye mitandao ya kijamii utachukuliwa kwa uzito kama ilivyo tu na uonevu wenye vurugu na unaweza kuwa sababu za kusimamishwa au kufukuzwa.

### *Vifaa vya Kuchezea, Vitu Binafsi na Simu za Mkononi:*

YouthCity itatoa shughuli, chakula, bidhaa na vifaa kwa washiriki wote. Hatuwajibiki kwa vifaa vya kuchezea au vitu vingine kama vile simu za mkononi, vifaa vya kuchezea au vichezaji mchezo vinavyobebeka vinavyoletwa kutoka nyumbani. Mpango wetu umeundwa kwa njia ambayo mtoto ana muda mdogo au haja ndogo ya kutumia kifaa cha mchezo au kicheza muziki kutoka nyumbani. Ingawa hatuwezi kuwakataza wanafunzi kuja na simu za mkononi kwenye mpango, tuna kanuni madhubuti kuhusu jinsi simu zinavyotumika katika mpango wetu. Sera yetu ni kwamba simu hazipaswi kutumika wakati wa masomo na wanafunzi watapewa onyo na kisha wataombwa kuzipeleka ofisini kwa muda uliosalia wa siku. Wazazi wanaweza kufikia wanafunzi wao kupitia namba yetu ya simu ya mpango na wanafunzi wanaweza kuwasiliana na wazazi kwa kutumia simu ya mkononi ya mpango inapohitajika.

Iwapo wanafunzi wataleta vitu binafsi kwenye mpango, tafadhali hakikisha kwamba ni bidhaa au vifaa ambavyo ni rahisi kutakaswa. Tunataka kuhakikisha kuwa tunafuata itifaki zote za usalama zilizowekwa na mpango. Hakuna vitu binafsi vinavyoweza kuachwa kwenye kituo usiku na wanafunzi wote wanatakiwa kupeleka nyumbani vitu vyote binafsi mwishoni mwa siku au vinaweza kutupwa.

### *Je, naweza kuja na nini kutoka nyumbani?*

Washiriki wote waojiandikishwa watapewa sehemu ya hifadhi na/au nafasi ya kuhifadhi vitu vyao binafsi. Ili kuhakikisha msimu wa kiangazi ulio salama na mafanikio tunapendekeza vijana walete vitu vifuatavyo vinavyoweza kuachwa kwenye kituo cha mpango kwa muda wote wa mwaka wa masomo.

- Mavazi ya kubadilisha yanayoweza kusalia katika YouthCity…endapo kuna dharura
- Shati ya rangi
- Mavazi ya msimu kama inavyohitajika

### *Sera ya Kuwasilisha Malalamiko:*

Iwapo mshiriki wa mpango, mzazi au mlezi ana wasiwasi kuhusiana na mfanyakazi au mpango wa Baada ya shule wa YouthCity au wa msimu wa kiangazi, utaratibu ufuatao wa kuwasilisha malalamiko unapaswa kutumika. Ikiwezekana, tafadhali jadili jambo hilo na Msimamizi Mkuu wa Mpango wa Jamii kwanza. Iwapo huwezi kujadili suala hilo na kiongozi wa mpango wa kituo chako, au hamjafikia suluhisho, tafadhali eleza wasiwasi wako kwa maneno au kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mshiriki wa Vijana na Familia. Mkurugenzi Mshiriki atawasiliana nawe ili kujadili matatizo pamoja nawe na wafanyakazi wanaohusika ili kutafuta suluhu. Ikiwa wasiwasi wako haujatatuliwa kwa njia inayokuridhisha, au ikiwa una wasiwasi kuhusu Mkurugenzi Mshiriki wa mpango, unaweza kueleza wasiwasi wako kwa maneno au kwa maandishi kwa Mkurugenzi wa Kitengo cha Vijana na Familia cha Salt Lake City. Mkurugenzi wa Kitengo atajadili suala hilo pamoja nawe na wafanyakazi wanaohusika ili kufikia suluhu. Ikiwa wasiwasi wako haujatatuliwa kwa njia inayokuridhisha, au ikiwa una wasiwasi kuhusu Mkurugenzi wa Kitengo, unaweza kuandika barua kwa Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Jamii na Mitaa ya Salt Lake City. Naibu Mkurugenzi atatoa uamuzi wa mwisho kuhusu jinsi suala hilo litakavyotatuliwa na kutuma barua ya majibu kwa mshiriki.

DIVISION *of*
**YOUTH & FAMILY**

## Mkataba wa Sera Dhidi ya Uonevu

**Kusudi**

Kitengo cha Vijana na Familia cha Jiji la Salt Lake kimejitoa kuhakikisha utu na usalama wa vijana wote unazingatiwa katika Jiji la Salt Lake. Sera hii inapiga marufuku uonevu, kushambuliwa, na kutishiwa katika huduma zote za jiji zinazohudumia vijana, shughuli, programu, na vituo ndani ya Kitengo cha Vijana na Familia cha Jiji la Salt Lake.

**Ufafanuzi**

"Kuonea" kutafafanuliwa kama kitendo au mwenendo wowote mbaya, ulioenea, au endelevu wa aidha kimwili, kielektroniki, au wa maneno ambao:

1. Unaweza kuwa na msingi wa asili ya kweli au inayodhaniwa ya kijana, rangi, kabila, dini, asili ya taifa, jinsia, umri, hali ya ndoa, mwonekano binafsi, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho au mwonekano wa kijinsia, uwezo wa kiakili, hali ya kifamilia, wajibu wa kifamilia, kudahiliwa chuo kikuu, kufungamana kisiasa, taarifa za kinasaba, ulemavu, chanzo cha kipato, au sifa nyingine yoyote tofauti, au kutegemeana na kuambatana kwa kijana na mtu au kundi lenye yoyote kati ya sifa za kweli au zilizodhaniwa zilizotajwa kabla; na

2. Bila shaka yoyote unaweza kutabiriwa:
    1. Kuwaweka vijana katika uwoga wa madhara ya kimwili kwa watu wao au mali zao;
    2. Kusababisha athari mbaya kwenye afya ya kimwili au kiakili ya kijana;
    3. Kwa kiasi kikubwa kuingiliana na ufaulu au mahudhurio ya kitaaluma ya kijana; au
    4. Kwa kiasi kikubwa kuingiliana na uwezo wa kijana kushiriki katika au kufaidika kutokana na huduma, shughuli, programu, vituo, au faida zinazotolewa na Kitengo cha Vijana na Familia.

**Marufuku dhidi ya Uonevu**

1. Vitendo vya uonevu, ikihusisha uonevu kwa njia ya mtandao, aidha na vijana, wanaojitolea, au wafanyakazi, vimepigwa marufuku katika huduma zote za jiji zinazohudumia vijana, shughuli, programu, na vituo.
2. Kisasi dhidi ya kijana, anayejitolea, au mfanyakazi anayeripoti uonevu, anayetoa taarifa kuhusu kitendo cha uonevu, au anashuhudia kitendo cha uonevu pia ni marufuku.
3. Huduma zote za Kitengo cha Vijana na Familia cha Jiji la Salt Lake, shughuli, programu, na vituo kwa ajili ya vijana vitaanzisha sera ya wazi kwa ajili ya kuripoti, kujishughulisha, na kuzuia uonevu kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Sera hii itahusisha hitaji la mafunzo ya mwaka kwa ajili ya wafanyakazi wote juu ya sera iliyosemwa na juu ya taratibu bora za kuzuia uonevu.